REVOLUTIONARY GOVERNMENT OF ZANZIBAR
MINISTRY OF TOURISM AND HERITAGE

ZANZIBAR TOURISM & INVESTMENT SHOW 2024

TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

ZANZIBAR YAANZISHA MAONESHO YAKE YA UTALII NA UWEKEZAJI

Uchumi wa Zanzibar umekuwa ukipitia katika mabadiliko makubwa sana huku sekta ya utalii ikiendelea kushamiri kutokana na ongezeko la wageni kwa kuimarika kwa urahisi wa usafiri kuja visiwani.

Sekta ya utalii inachangia 30% ya Pato la Taifa na zaidi ya 80% ya upatikanaji wa fedha za kigeni. Uwekezaji katika sekta ya utalii umeongezeka na unatarajiwa kuendelea kuongezeka zaidi kupitia nyanja tofauti kutokana na bidhaa za utalii zilizoandaliwa na Kamisheni ya Utalii. Idadi ya wageni walioingia Zanzibar kwa mwaka 2023 imefikia 638,498, sawa na ongezeko la 16.4% ikilinganishwa na 548,503 walioingia mwaka 2022. Zanzibar ina matarajio makubwa zaidi ya kuongezeka kwa wageni na hasa kupitia uzinduzi wa safari mpya za ndege mwishoni mwa Juni, Julai na Agosti na ikizingatiwa kuwa miezi hiyo ni msimu mkubwa wa utalii Zanzibar.

Kwenda sambamba na kukua kwa kasi hii kubwa ya maendeleo ya Zanzibar, inaifanya Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale kwa kushirikiana na Kamisheni ya Utalii Zanzibar, kutangaza rasmi Maonesho ya kwanza ya Utalii na Uwekezaji hapa Zanzibar yanayotarajiwa kufanyika mwezi wa Oktoba mwaka huu 2024.

Tukio hilo la kipekee katika sekta ya utaliii litakuwa ni la aina yake katika historia ya Zanzibar, na litakuwa ni jukwaa kuu la kuonyesha fursa za kiutalii na uwekezaji Zanzibar. Chini ya kaulimbiu **“Kukuza Utalii Endelevu, Uhifadhi wa Urithi na Uwekezaji,”** maonesho haya yatafanyika katika Kituo cha Maonesho cha Zanzibar - Dimani kuanzia tarehe 25 na 26 Oktoba 2024. Tukio hili la kusisimua na litakuwa ni jukwaa la kimataifa la kuonyesha Zanzibar, utamaduni wake uliohai, na uwezo wake mkubwa wa uwekezaji, kuvutia watalii, wawekezaji, na wataalamu wa sekta kutoka Tanzania, Afrika na duniani kote.

Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale imeandaa mikakati ya kuonyesha umuhimu wa tukio hili kubwa katika kuifanya Zanzibar kuwa juu kwa utalii na uwekezaji endelevu, kutokana na wageni kupata fursa ya kusafiri na kuwa uelewa wa kutosha kuhusu uhifadhi wa mazingira. Wizara inasisitiza kuwa maonesho haya ni hatua muhimu sana katika kuiweka Zanzibar kwenye ramani ya dunia kama eneo lenye fursa za kipekee za kuwekeza katika visiwa vyake vya Unguja na Pemba.

Kamisheni ya Utalii Zanzibar inaendelea kusisitiza dhamira zake mbili za tukio hili, ikiwa ni kusherehekea urithi na utamaduni wa Zanzibar pamoja na kufungua hazina za zamani ili kuweza kuleta fursa zisizo na kikomo katika siku zijazo. Katika kukuza uelewa wa kina wa historia na mila zetu, tumejikita kutoa elimu ya njia bora za uwekezaji endelevu unaolenga kuzinufaisha jamii zetu na kuhifadhi utambulisho wetu wa kipekee.

Utalii wa Mikutano na Maonesho (MICE) ni miongoni mwa maeneo ya kipaumbele cha masoko ya Kamisheni ya Utalii. Kutokana na ongezeko kubwa la Utalii wa huo, Kamisheni ya Utalii ina lengo la kuandaa njia zake za kipekee za kukuza utalii huo hapa Zanzibar. Maonesho haya yatakuwa na wadau wa Utalii zaidi ya 250 wa hadhi ya juu, ikiwa pamoja na waandaaji wa misafara ya kitalii, wamiliki wa miradi mikubwa ya kitalii kama hoteli pamoja na vivutio vya Utalii kutoka Zanzibar, Tanzania, Afrika Mashariki, na duniani kote.

REVOLUTIONARY GOVERNMENT OF ZANZIBAR
MINISTRY OF TOURISM AND HERITAGE

ZANZIBAR TOURISM & INVESTMENT SHOW 2024

Maonesho hayo yatavutia, na kutoa nafasi nzuri kwa wawekezaji na kutoa maarifa ya kina kuhusu soko la Zanzibar kupitia warsha na semina za kipekee zitakazokwenda sambamba na Maonesho hayo. Washiriki watapata fursa ya kujionea maendeleo mapya ya soko, maeneo mapya, na bidhaa mpya za kitalii ambazo zinaweza kuongeza thamani kubwa kwenye orodha zao za uwekezaji na kutoa uzoefu wakipekee kwa watalii na wageni.

Zanzibar ina fursa nyingi za uwekezaji kutokana na urithi wake wakipekee wa utamaduni wake mzuri wa asili. Maonesho haya yatatoa fursa za kipekee kwa wawekezaji katika sekta ya utalii na ukarimu. Washiriki watakutana na wamiliki wa miradi, na taasisi zote za ndani kuelewa njia za uwekezaji unaolenga kunufaisha nchi nzima. Maonesho ya Utalii na Uwekezaji Zanzibar 2024 yataleta mwanga wa utalii endelevu pamoja na fursa za uwekezaji wenye tija na uhai. Lengo ni kuweka kumbukumbu za kudumu na kuchangia katika kutunza. kuhifadhi na kuboresha utamaduni wa Zanzibar, Tanzania, Afrika Mashariki, na duniani kote.

Kwa maelezo zaidi, tembelea **www.zanzibartourismshow.com**

Supported by

ZIPA
HAZ HOTEL ASSOCIATION ZANZIBAR
ZATI Zanzibar Association of Tourism Investors
ZATO
ZATOGA
ZNCC Zanzibar National Chamber of Commerce